## Utakatifu Kwake Mungu

# Ningependa Maovu

## By Rev. George Leon Pike Sr.

Ujumbe huu umeandikwa kwa kupeana bure bila malipo yoyote. Kwa nakala zaidi andika kwa kingereza ikiwezekana kwa anwani iliyoko chini ukieleza ni nakala ngapi unaweza kutumia vizuri.

**Published By**

**Grace Temple**
**PO Box 511**
**Monroe, GA 30655-0511 USA**
**Web: www.GraceTempleOnline.org**
**Email: info@GraceTempleOnline.org**

**SWA9907 • Swahili • Fear No Evil**

http://www.transology.info/tracts/swa9907t.htm

# Ningependa Maovu

Ningependa kwanza somo letu na mojadiliano kwa kuuliza swali lili: kweli una turaha, amo umefungwa kiroho kwa mawazo na uoga? Unajua, kuna watu wengi ambao hujifanya kwamini kwamba wana furaha, lakini nimegundua, kama mhubiri au mhuduma, kwamba wengi hawana furaha ya kweli. Na nina sismkuo kueleza kwa undani ukweli wa uzima. Tunaambiwa na mmoja wa waandishi mashuhwi wa Bibilia, kwamba wakati Kristo, ambaye ndiye uzima wetu, anapo onekana, ndipo tunapoanza kwishi.

Watu wanapozaliwa duniani bumu, wanazaliwa katika kifo. Wamekuja humu duniani kwa lengo moja, na hilo ni kufa. Paulo alisema katika maandiko, kwamba maisha yetu yote, tuko jini ya ufungwa, kwa sababu ya hofu ya kifo; lakini unajua. Kwamba mtu akizaliwa katika ufalne wa Mungu, amezaliwa katika uzima, ili aishi mahali pa ukweli. Hana hofu ya kifo, kwasababu amepita kutoka kwa kifo hadi kwa uzima. Bwana anataka watu waishi kwa uzima bila hofu. Anatueleza katika Neno lake kwamba tusiache mioyo yetu kusumbuliwa.

Na hapo, bile shaka, tunafahamu kwamba tuna uwezo kuweka mioyo yetu kutosumbuka. Haino maena kwetu kumuita Mungu na kumwomba atutundee jambo, ambalo, sisi wenyewe, tunaweza; ila tuombe kuwa na uwezo wa kutenda yale Mungu anataka tutende. Njia ya mioyo yetu kutusumbuka na hofu ya maisha ni kuwa na Imani katika ahadi za upendo na za uza: dizi kutoka kwa Mungu, na tuweke matumaini yetu yote katika Mungu, tukimwamini na moyo wote. Naye atatimiliza.

Daudi alisema, “Sitaogapa maovu”. Yesu anatuambia katika neno lake, “Wala mioyo yenu isifadhaike”. Mungu hakutupatia roho wa hofu. Hofu ni ya shetani Tusiogope hata umasikini, kwa maana umasikini ni maovu. Na kuogopa umasikini ni kutokuwa na imani katika neno la Mungu, kwa maana Alisema anapenda kwa kilejambo tufanikiwe na kuwa na afya, jinsi roho zetu zifanikiwavyo.

Kuto amini ni kutomfurahisha Mungu. Kisicho cha imani ni cha dhambi, tunatakaswa kwa imani ana tunaokolewa kwa neema kupitia imani. Kuogopa magonjwa ni kutoamini neno la Mungu, kwa maana maandishi yanasema, “Mimi ni Mungu wako, akusameheaye maovu yako yote na akuponyaye magonjwa yako yote”. Kumtuka, tusiogope kuanguka ama dhambi. Tunaambiwa ameshaponya kutelesa kwetu, na hakuna chochofe kinechoweza kututenga na mapenzi ya Mungu. Hata Shetani hana nguvu kututenga. Lazima wewe, kwa tamaa zako, upinduke na umuwache Mungu. Ukitanya haya, kwa sababu shetani anakujaribu kutamani na kutenda dhambi, inaonyesha waz, kulingana na Bibilia hujamwona Mungu kata humjui. Hivyo, tunaona ulinzi wa milele ndani yake. Utapoteza upendo wa dunia hii na yote yaliyamo mara mtu wa kale apapokufa, na mtu mpya, amevaa Kristo, anapenda mambo ya mbiguni. Masungumzo yake ni matakatifu, yeye ni kiumbe kipya. “Tazama, yakale yamepita, na mambo yote yamekuwa mapya”. Bibilia husema.

Daudi wa kale alisema, “Nilimfafute Mungu na akanisikia, na alinikomboa kutoka kwa hofu yangu”. Mbona unawache shetani kuleta mawazo katika tikira na moyo wako, kufanya imani yako kuogapa, kusumbuka na kutaamini? Na aendelee kukufinya zaidi ya fikira zako. Mungu alisema, “Sitakuaclilia ucharibiwe zaidi ya hapo unaweza kustahimili, lakini nitaweza kwa kila jaribio kufungwa njia ya kutoka” ili uweze kustahimili. Anatuambia tulete jini kila mawazo na kila jambo kuti, kwa imani na tuamini katika neno lake.

Kataa kujisikia kwako, na kataa fikira zako. Nena na fikiria neno la Mungu! Ishi neno! Penda neno! Ongea kuhusu neno! Imba neno! Aachilia liwe hitaji la moyo wako, na unapoachilia fahamu zako kwa Kristo Yesu, utakuwa na amani iliyo kamilika. Hakuna amani kwa waovu. Alisema tunatakaswa kwa Imani katika neno lake, hivyo. Vile Yesu alisema, “Usiogope!”

Wewe kuogopa nguvu zozote zilio kinyume ni wewe kuwa jini ya nguvu hizo, na zinafanyika bwana kwako na zinakupanya mfungwa.

Imeandikwa na Rev. George Leon Pike Sr.

Yeye alianzisha “Jesus Christ’s Eternal Kingdom of Abundant Life, Inc.”

Utakatifu Kwake Mungu